

*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Ajira na Mahusiano Mhe. Deus Sangu akifuatilia maelezo ya Kijana Mnufaika wa Mafunzo ya Uanagenzi Fani ya Ufundi Bomba, Ismail Mbogo alipotembea Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST), kampasi ya Rukwa.*

# e-GA: MIFUMO YA KIDIGITALI YA KILIMO INAONGEZA UWAZI

Na Aziza Masoud,
***DODOMA***

SERIKALI kupitia Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) inaendelea kushirikiana na Wizara ya Kilimo katika kuimarisha matumizi ya mifumo ya kidijitali inayorahisisha utoaji wa huduma, kuongeza uwazi na kuboresha usimamizi wa shughuli za kilimo nchini.

Akizungumza jana katika Maonesho ya Wakulima ya Kitaifa yanayoendelea jijini Dodoma, Meneja wa Mawasiliano e -GA Subira Kaswaga alisema taasisi hiyo imeshiriki katika ujenzi wa mifumo mbalimbali ya sekta ya kilimo, ikiwemo mfumo unaowezesha Wizara ya Kilimo kupata taarifa za wakulima nchini, kufuatilia shughuli za taasisi zilizo chini ya wizara hiyo na kutoa taarifa muhimu za kilimo kwa wadau.

Aliongeza mamlaka hiyo imeshirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika kutengeneza mfumo wa usimamizi wa vyama vya ushirika unaojulikana kama MUVU, unaosaidia kuongeza uwazi katika uendeshaji wa vyama hivyo pamoja na kuwawezesha wakulima kufuatilia mauzo ya mazao yao, bei na malipo wanayostahili kupata.

"Hadi sasa zaidi ya vyama 6000 vya ushirika vinatumia mfumo huo, jambo lililosaidia kuboresha usimamizi wa mapato na kuongeza uwajibikaji katika sekta ya ushirika.

Alisema mamlaka hiyo ina jukumu la kuandaa na kusimamia mifumo mbalimbali ya TEHAMA inayotumika serikalini ili kuboresha utendaji kazi wa taasisi za umma na kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi.

Alieleza kuwa e-GA imeshirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) kuanzisha Fertilizer Information System (FIS), mfumo unaowezesha kusimamia wazalishaji na waingizaji wa mbolea, kufuatilia mwenendo wa soko na kuhakikisha wauzaji wanazingatia bei elekezi zinazotolewa na Serikali.

Alisema mfumo huo unaisaidia Serikali kudhibiti soko la mbolea ili wakulima waweze kupata pembejeo hizo kwa bei stahiki na hivyo kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao.

Mbali na mifumo hiyo, taasisi za sekta ya kilimo zinaendelea kutumia mifumo mingine ya Serikali ikiwemo barua pepe za Serikali (Government Email System) na Mfumo wa Ofisi Mtandao, ambayo imeboresha mawasiliano na utendaji kazi ndani ya taasisi za umma.

Mamlaka hiyo imewataka wananchi kutembelea banda la e-GA katika maonesho yanayoendelea Dodoma ili kujifunza zaidi kuhusu mifumo ya kidijitali inayotumika kuboresha utoaji wa huduma za Serikali na mchango wake katika maendeleo ya sekta ya kilimo.

# DK.MWIGULU AITAKA TADB KUPANUA WIGO WA MIKOPO YA WAKULIMA

Na Aziza Masoud,
***DODOMA***

WAZIRI Mkuu Dk.Mwigulu Nchemba ameiagiza Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kupanua huduma za utoaji wa mikopo kwa lengo la kuwafikia wakulima, wafugaji na wavuvi wengi zaidi nchini ili kuweza kusaidia uwekezaji katika sekta ya uzalishaji na kuharakisha mageuzi.

Dk.Mwigulu ametoa kauli hiyo jijini Dodoma katika Maonesho ya Taifa ya Wakulima Nanenane baada ya kutembelea banda la benki ya TADB na kuwa benki hiyo imeendelea kuwa chombo muhimu cha Serikali katika kuwezesha uwekezaji kwenye sekta za kilimo, mifugo na uvuvi kwa kutoa mitaji kwa wakulima, wafugaji, wavuvi na wawekezaji mbalimbali.

Alisema hatua hiyo iende sambamba na kujiimarisha katika uwezo wa kifedha kwa lengo la kuwafikia wakulima, wafugaji na wavuvi wengi zaidi nchini ambapo itasaidia kuongeza uwekezaji katika sekta za uzalishaji.

Alisema pia itasaidia kuharakisha mageuzi ya kilimo, mifugo na uvuvi, kuongeza tija na uzalishaji, sambamba na kuimarisha uchumi wa taifa kupitia sekta hizo zinazobeba maisha ya Watanzania wengi.

Alisema ili Tanzania ifikie malengo ya kuongeza uzalishaji wa mazao na kuhakikisha usalama wa chakula nchini, kuna umuhimu wa kuendelea kuiwezesha TADB kifedha ili iweze kukidhi mahitaji yanayoongezeka ya wakulima na wadau wengine wa sekta ya kilimo.

" Serikali haiwezi kutegemea ruzuku pekee kila mwaka katika kuendeleza sekta ya kilimo, hivyo taasisi za kifedha kama TADB zina wajibu mkubwa wa kuhakikisha mitaji inapatikana kwa wakati kwa wakulima, wafugaji na wavuvi,"alisema Dk.Nchemba. Alisema kuwa benki hiyo inapaswa kuongeza uwezo wa kufadhili ununuzi wa mbolea, pembejeo, zana za kisasa za kilimo pamoja na miradi ya kuongeza thamani ya mazao ili kuongeza tija, ushindani na thamani ya bidhaa za Tanzania katika masoko ya ndani na nje ya nchi.

Naye Mkurugenzi Mwendeshaji wa benki ya TADB, Frank Nyabundege, amesema benki hiyo imeendelea kufadhili miradi mbalimbali ya kimkakati inayochochea ukuaji wa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi nchini.

# BRELA YAHAMASISHA WANANCHI KURASIMISHA BIASHARA MAONESHO YA NANENANE DODOMA

Na Mwandishi Wetu,
***DODOMA***

WAKALA wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) umewataka wafanyabiashara, wakulima na wananchi kwa ujumla kutumia Maonesho ya Nanenane yanayoendelea katika viwanja vya Mzunguni, Dodoma, kupata huduma mbalimbali za urasimishaji wa biashara pamoja na elimu kuhusu mfumo mpya ulioboreshwa wa usajili.

Akizungumza juzi katika maonesho ya Nanenane, Afisa usajili wa BRELA, Yusuph Mwasakafyuka Regio, alisema taasisi hiyo inatoa huduma katika banda la Wizara ya Viwanda na Biashara kuanzia Agosti 1 hadi Agosti 8, ambapo wananchi watapata huduma ambazo kwa kawaida huzipata katika ofisi za BRELA.

Alizitaja huduma hizo kuwa ni usajili wa majina ya biashara, usajili wa kampuni, utoaji wa leseni za biashara Kundi A, utoaji wa leseni za viwanda pamoja na usajili wa awali wa alama za biashara (Trademark).

"Tunawahamasisha wafanyabiashara, wakulima na wananchi wote kufika katika banda la BRELA ili kupata huduma hizi kwa urahisi na kuendelea kurasimisha shughuli zao za kiuchumi. Kilimo cha sasa ni kilimo biashara, hivyo ni muhimu shughuli hizo zikafanyika kwa kuzingatia taratibu za kisheria," alisema.

Aidha, alisema BRELA imeboresha mfumo wake wa usajili ili kuongeza ufanisi na kurahisisha utoaji wa huduma kwa wateja, huku ikiondoa changamoto zilizokuwapo katika mfumo wa awali wa ORS.

Alieleza kuwa kupitia mfumo huo mpya, huduma ambazo awali zilihitaji mteja kufika ofisini sasa zinaweza kufanyika kwa njia ya mtandao, ikiwemo uwasilishaji wa taarifa za dhamana (charges) zinazohusisha mikopo kutoka taasisi za fedha.

Kwa mujibu wake, mfumo huo pia umeongeza uwazi kwa kuwawezesha wananchi kupata taarifa za kampuni kwa urahisi zaidi, ikiwemo hali ya uwasilishaji wa taarifa za mwaka (annual returns), jambo ambalo halikuwa rahisi katika mfumo wa zamani.

Pia alisema maboresho hayo yameimarisha usalama wa taarifa za kampuni kwa kuhakikisha wanahisa na wakurugenzi wanapokea taarifa kila mabadiliko yanapofanyika ndani ya kampuni husika, hatua inayolenga kuzuia mabadiliko yasiyofanywa kwa ridhaa yao.

Alifafanua kuwa ili kutumia mfumo huo mpya, mwananchi anatakiwa kuwa na Namba ya Utambulisho wa Taifa (NIN), namba ya simu inayotumika pamoja na anuani sahihi ya barua pepe.

BRELA ni taasisi inayosimamia utekelezaji wa sheria mbalimbali za urasimishaji wa biashara nchini, ikiwemo usajili wa makampuni, majina ya biashara, alama za biashara, leseni za biashara Kundi A na leseni za viwanda.